

# RIZIKI



Desemba/2023 - Februari/2024

**YESU KRISTO**

**NI NJIA YA UZIMA**

**TOLEO  
LA  
4/2023**



## RIZIKI

S.L.P. 2696, Arusha  
0759 544 917  
Barua pepe:  
editor.somabiblia@gmail.com

### Kamati ya Riziki:

James Sabuni (mhariri)  
Mch. Anza Amen Lema  
Mch. Philip Bach-Svendsen  
Cathbert Msemo  
Mary Bura  
Magreth Mushi  
Mch. Gervas Meitamei  
Luhekelo Sanga

### Waandishi walioshiriki:

Mch. Gideon Mumo  
Agape T. Mnzava

### Layout:

Cathbert Msemo

### Jalada:

Cathbert Msemo

ISSN 2683 - 6491

Nakala: 5000

### Usambazaji:

## SOMA BIBLIA

S.L.P. 2696, Arusha  
S.L.P. 12772, Dar es Salaam  
S.L.P. 1088, Iringa  
S.L.P. 6097, Mwanza  
S.L.P. 1062, Mbeya  
S.L.P. 423 I, Dodoma

www.somabiblia.or.tz

Neno la Injili  
kwa rika zote  
Tanzania!

Imechapwa na:  
Imaging Smart - Dar es Salaam

## Kuna njia moja tu

Katika ulimwengu wa leo kuna njia nyingi za kutumaini. Hutokana na kuwepo kwa dini nyingi, na wingi wa mitazamo na mawazo yanayotofautiana juu ya furaha ya milele na Mbinguni. Na kila mtu huamini ya kuwa amesimama katika ukweli kuhusu tumaini la furaha ya kudumu.

Wengi wetu wanapenda kuishi katika dunia hii kwa muda mrefu iwezekanavyo. Tena wengine wanatamani wangeishi milele katika dunia hii.

Mada kuu katika toleo hili la nne la Riziki 2023 ni *Yesu Kristo ni njia ya uzima*. Kuna njia nyingi, lakini tunakumbushana kuwa kuna njia moja tu ya kumwingiza mtu katika furaha ya kweli ya milele. Kuna ukweli mmoja tu umfanyao mtu kuwa huru. Kuna namna moja tu ya maisha itakayomfikisha mtu katika uzima wa milele. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ndiye Njia hiyo moja.

Kwa nini tuamini hivyo? Kwa sababu Yesu ndiye Kweli. Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu. Tena ndiye Uzima. Alifufuka kutoka kwa wafu. Yeye pia ndiye atakayewahukumu watu wote siku ya mwisho.

Katika toleo hili utakutana na habari ya mtu mmoja ambaye aliamua kupita njia ambayo kwa desturi za kwao hakutakiwa kupita. Uamuzi wake wa kufanya hivyo ulileta mabadiliko makubwa katika jamii ile. Utapata pia mafundisho na shuhuda za kukusogeza karibu na Mungu. Kumbuka Yesu alivyotambua, "*Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi*" (Yn 14:6). Hivyo tumfuate yeye aliye njia.

James Sabuni

## Yaliyomo:

- Uk. 3-4: Yesu Kristo ni njia ya uzima
- Uk. 5-7: Teknolojia na familia
- Uk. 8-9: Mwanamke Msamaria
- Uk. 10-11: Nimerudi na makovu, tena mtupu
- Uk. 12-13: Bwana Anakuja
- Uk. 14-16: Anza yote na Bwana

## Yesu Kristo ni njia ya uzima

Maisha yetu ya kawaida yanahitaji kwa-mba tunachagua na kufuata uelekeo fulani. Ni muhimu kujua unapotaka kwenda na njia ya kukufikisha. Neno la Mungu linatukumbusha kuwa Yesu Kristo ni njia ya uzima. Katika Yn 14:6 Yesu anasema, "*Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu.*" Yaani sisi Wakristo hatuwezi kufika Mbinguni bila ya kwenda njia hii ambayo ni Yesu Kristo. Yeye ndiye njia pekee ya uzima wa milele.

Sisi tunapomwamini na kumfuata Yesu Kristo tunaishi maisha ya ushindi. Neno lake linatuongoza katika kumwelewa zaidi Mungu na uhuru wa kuishi kwenye uweza wake. Yesu anasema, "*Kama mkidumu katika maneno yangu, mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka huru*" (Yn 8:31-32). Tunaangalizwa kuwa mafundisho ya Yesu Kristo pekee ndiyo yanayotuletea uelewa na ufahamu wa kweli katika maisha yetu.

### Upekee wa Yesu Kristo

Neno la Mungu katika vifungu mbalimbali linathibitisha kuwa Yesu Kristo ndiye njia pekee ya kutufikisha Mbinguni. Yesu Kristo ndiye aliyeteuliwa na Mungu awe mwokozi wetu (1 Pet 2:4). Yeye pekee ndiye aliyefanikiwa kuishi maisha makamilifu yasiyo na dhambi (Ebr 4:15). Yeye pekee ndiye dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu (1 Yoh 2:2; Ebr 10:26). Yeye pekee ndiye aliyekamilisha Torati ya Mungu na kile walichonona manabii (Mt 5:17). Yeye ndiye mtu pekee aliyeshinda mauti milele (Ebr 2:14-15). Yeye pekee ndiye Mpatani-

shi wetu kwa Mungu (1 Tim 2:5).

Maishani mwetu tunahitaji sana uwe-po wa Mungu. Musa alitaka utukufu na uthibitisho wa uwepo wa Mungu. Akamwambia Mungu amjulishe ni nani ambaye Mungu atamtuma pamoja naye. Mungu anamwambia atakwenda pamoja nao. Musa anaendelea kung'ang'ana na BWANA: Uniambie, nani atakwenda nasi? Na hapo Mungu anamwambia, "*Uso wangu utakwenda pamoja nawe, nami nitakupa raha*" (Kut 33:14). Musa alitambua kuwa uwepo wa Mungu ndio kila kitu (Kut 33:16). Kumbe, itakuwa upumbavu kujaribu kwenda bila Mungu (Zab 53:1).

Uzima wa milele kule mbinguni wawezekana tu kupitia Kristo. Neno la Mungu linasema kwa maneno ya Yesu, "*Uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma*" (Yn 17:3). Ili kupokea wokovu, kama zawadi ya bure toka kwa Mungu, ni lazima tumtazame Yesu Kristo, na Yesu peke yake. Ni lazima tupokee kwa imani kile kifo chake kwa ajili yetu pale msalabani kama malipo ya dhambi zetu, na kujihesabu kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu kutokana na ufufuo wake (Rum 6:11). "*Ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio*" (Rum 3:22).

### Tunakwenda njia iliyo hai?

Kuna wakati katika huduma ya Yesu ambapo makundi ya watu yalimtelekeza na kujitenga naye. Hawakuwa na tu-



maini tena kwamba atakuwa mwokozi yule waliyetazamia kuja kwake. Na Yesu akawauliza wale Thenashara (Yn 6:67), "Je! Ninyi nanyi mwataka kuondoka?" Petro akamjibu Yesu kwa usahihi kabisa, "Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. Nasi tume-sadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu" (Yn 6:68b-69). Sisi nasi tutafute kuwa na imani sawa na Petro kwa kutambua kuwa uzima wa milele wapatikana kwa Kristo peke yake.

Yesu Kristo ni njia ya uzima wetu. Siyo tu alikuja dunia kimwili ili kutuone-sha njia, hata yeye mwenyewe ndiye njia hiyo. Alikuwa kutukombo. Kumfuata humaanisha zaidi ya sisi kutembea alivyotembea. Humaanisha kumtegemea Yesu tukiamini "nija ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake" (Ebr 10:19). Tunaagizwa kufuata nyayo zake, na kuishi kama alivyoishi. Lakini kwanza na hata mwisho tunambiwa kumtegemea kwamba mwili wake, aliutoa kama sadaka kwa ajili ya dhambi zetu, ndio njia hiyo mpya inayotufikisha kwa Mungu. Na tunaweza kuienda kwa ujasiri, mwandishi wa Waraka kwa Waebrania anaongeza (Ebr 10:22; 4:14-16).

Kwenda njia humaanisha kwamba tu-

nasonga mbele. Tunapomfuata Yesu kwa imani ni sambamba na kuelekea mahali alipotuandalia makao ya kudumu. Kwa sababu ya ahadi ya Yesu na jinsi alivyofanya kwa niaba yetu, tunakuwa na uhakika kwamba muda wetu hapa duniani utakapoisha, tutaenda katika uzima wa milele.

### Uzima wa milele

Yesu anatumkumbusha pia kuwa "si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakaye-ingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni" (Mt 7:21).

Kwa hiyo sisi sote tunahimizwa kutafuta uwepo wa Mungu na kuukaribisha katika maisha yetu. Nao unadumu kuwa pamoja nasi tunapomfuata Yesu Kristo. Tumpe nafasi katika nyanja zote za maisha yetu, ili kila tulifanyalo tulifanye kwa jina la Yesu Kristo.

Hapo ndipo tutakuwa na mafanikio endelevu katika maisha yetu, maana Yesu ndiye njia ya kweli ya uzima. Tukitoea ki-paumbele kwa kujifunza kwake hatutakosa huo uzima ambao ni wa milele, kwa sababu ndio huu wa kumjua Mungu wa pekee wa kweli na Yesu Kristo aliyetumwa naye ili kuturudisha kwa Mungu.

.....  
Mch. Anza Amen Lema

## Teknolojia na familia

Teknolojia mpya ni kitu kinachoathiri maisha yetu ya kifamilia siku hizi. Kwa muda wa miaka michache maarifa yameongezeka sana ya kutumia sayansi na ufundi katika mitambo na zana za viwanda na kilimo, lakini pia jikoni na kwa namna zetu za kuwasiliana.

### Tumeumbwa wenye ubunifu

Mungu alituumba na hali ya udadisi na uvumbuzi wa mambo. Hali hiyo ilikuwa itusaidie kwa ajili ya kuilima na kuitunza bustani ile walimowekwa wanadamu wa kwanza.

Baada ya mwanadamu kumwasi Mungu tunaona kwamba watu waliendelea kutumia uwezo huo wa kuunda teknolojia kwa njia mbili:

Henoko, kwa mfano, alijenga mji mbali na Mungu (Mwa 4:16-17), na mnara mrefu katika nchi ya Shinari ulijengwa kwa lengo la wajenzi kujifanyia jina badala ya kulisifu jina la Bwana (Mwa 11:4).

Kwa upande mwingine, mafundistadi waliojenga kwanza hema ya kukutania na baadaye hekalu la Yerusalemu walitumia pia teknolojia yote iliyofahamika wakati ule ili kumfanyia Mungu nyumba iliyopendeza sana, na Mungu aliwabariki kwa kuwajalia hekima, maarifa na ujuzi mwingi (Kut 31:3-4).

Kwa hiyo fundisho la msingi kuhusu teknolojia ni kwamba si suala la teknolojia yenyewe, kama ni nzuri au mbaya, bali tujipime wenyewe jinsi tunavyoitumia. Je, tunaipokea kwa shukrani kwa Muumba wetu aliyetuwezesha kuiunda, na kumwomba atusaidie kuitumia kwa ajili ya kulisifu jina lake, kuwaleta watu karibu

na Kristo Yesu na kuboresha maisha yao?

Nyakati zinabadilika, na hali zinabadilika, lakini sheria za Mungu zinakaa milele. Dunia inabadilika kwa kasi sana, lakini Neno la Mungu linadumu milele. Mungu atusaidie kulifuata hilo tukiendelea kujadiliana jinsi tuwezavyo kutumia vema teknolojia mpya katika familia zetu.

### Athari za mabadiliko ya teknolojia

Teknolojia mpya siku hizi imekuwa na faida kubwa sana kwa jamii zetu. Imerahisisha mambo mengi. Kwa mfano, tiba na njia za kutoa tiba zimeboreshwa sana kuliko mwanzo. Kuna teknolojia nyingine zinazowezesha ufukishwaji wa taarifa na mawasiliano kwa haraka, na kuboresha usafiri, usafirishaji na upatikanaji wa elimu katika ngazi zote.

Faida moja ingekuwa kwamba tutapata muda mwingi kwa kuwa pamoja kama familia, siyo? Lakini hali halisi inasemaje? Kwa mfano, teknolojia mpya ya mawasiliano, je, tunaitumia kwa ajili ya kwenda huko na huko 'tukizungumza' kwa njia ya simu tu badala ya kukaa pamoja na kuongea bila zana kutuunganisha?

Tukumbushane tena, athari hasi nyingi hazitokani na mabadiliko ya kiteknolojia, bali na sisi wenyewe kushinda kudhibiti matumizi yake. Hatua moja katika kufaulu ingeweza kupatana kwamba wote wanazima simu muda wa kukaa pamoja kifamilia. Pengine si rahisi kutulia mara ya kwanza, lakini baada ya kuzoea hali hiyo kidogo wote watatazamia na kufurahia vipindi hivi; na tumshukuru Mungu, dunia haitaangamia kwa sababu ya kuzima simu.

### Maarifa kupita kiasi

Mhubiri anasema kuwa “aongezaye maarifa huongeza masikitiko” na katika wingi wa hekima mna wingi wa huzuni na kujilisha upepo (Mhu 1:17-18). Je, si kupinga kwamba maarifa ni mazuri?

Kuna mambo mawili hapa ya kuzingatia: Kwanza, Mhubiri anazungumzia faida ya kazi yote ambayo mtu anaifanya “chini ya jua” kana kwamba mambo ya dunia hii ni yote (Mhu 1:3). Lakini ni Mungu peke yake, Mungu mwenyewe, awezaye kutuliza mioyo yetu na kutupa kujisikia kuwa na amani na furaha. Hutukumbu-sha umuhimu wa sala za kifamilia.

Pili, sisi wanadamu tumeumbwa tukiwa na mipaka, pia kwa upande wa kupokea maarifa na kufaidika nayo. Siku hizi intaneti na kipekee mitandao ya kijamii inatupa habari mpya kwa kiasi na kasi tusivyoweza kumudu. Urahisi wa kuona mambo mengi yanayohusu maisha ya watu wengi duniani umekuwa majaribu kwetu kuvuka mipaka yetu ya kimwili. Si afya. Kama tukikubali kutafuta kujipatia habari mpya zote zinazorushwa kwa njia yoyote, tutakuta kwamba tunaongezewa masikitiko na hata kuchanganyikiwa.

### Thamani ya wakati

Katika Mhu 3:1-8 Mhubiri anaonyesha umuhimu wa wakati. Kila jambo limewekwa na Mungu katika mpango wa wakati.

Hatua ndogo katika kudhibiti kuongezeka kwa uwezo wa kuona na kusikia kwingi, kwa mfano kwenye mitandao ya kijamii, ni kujipatia muda fulani tu kila siku kwa ajili ya kuwa ‘online’. Sasa huenda utajikuta kwamba leo

hii muda wako umekwisha na unaweka simu pembeni, lakini hujui jinsi ya kufanya ila kushika tena simu na kuiwasha, maana unajisikia ni ‘boring’ kukaa hivihivi tu, basi ujue kwamba mapumziko haya ni baraka kwa akili yako. Mapumziko ni ya lazima, kwa sababu bila hayo akili yako itakosa muda muhimu kwa ajili ya kupanga kumbukumbu ya habari zile nyingi ulizopokea tayari.

### Kupoa kwa upendo

Paulo anaonya kwamba “siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari” (2 Tim 3:1). Tuko Wakristo wengi tunaajisikia kuishi katika wakati wa aina hiyo, na tunalaumu utandawazi na teknolojia kwa sababu ya upendo kupoa na amani kutoweka.

Lakini watu wakijisikia wapweke, si kwa sababu teknolojia imeondoa ukaribu wa jamii. Kwa kweli, imeongeza ukaribu. Ila sisi tumeitumia vibaya kwa ajili ya kujipenda wenyewe kuliko kupendana sisi kwa sisi, tena tumekuwa wapendao anasa ile inayopatikana kwa njia ya teknolojia mpya kuliko kumpenda Mungu.

Fikiri kidogo jinsi unavyoweza kutumia simu yako kwa kumtia moyo mtu unayejua anaweza kujisikia mpweke, kisha itumie hivyo badala ya kuangalia YouTube.

Pengine unajaribiwa kutazama picha na video za uchi kwenye intaneti. Uwe na Biblia kwenye simu yako, na kila unapajaribiwa, badala ya kwenda mtandaoni, tafuta kufungua Biblia hiyo ukimwomba Mungu akufumbue macho yako uya-tazame maajabu yatokayo katika neno lake.

Je, unakumbuka jinsi tulivyotumi-ana kadi za salamu za Krismasi na kwen-nda kutembeleana? Badala ya kulaumu teknolojia, tumia jinsi teknolojia ilivyo-boresha usafiri ili uende kumwona mmoja ambaye unajua utamfurahisha sana ukitokea kwake.

Si ajabu kuna familia zimetembeleana, lakini wanapokaa pamoja kila mmoja yuko kwenye simu akichati. Kama ni picha ya familia yako, uwe wa kwanza kumpendekea kwamba mtaimba pamoja, kufanya mchezo na kuwa na matembezi ya pamoja. Uwezekano upo kwamba badala ya kupoa, hata upendo utahuishwa kwa njia hizo!

### Kufundishana

Pengine tunaona tuna hali ngumu kama wazazi kwa sababu ya kububujika kwa teknolojia mpya kila wakati. Lakini tukumbuke kwamba watakaishi nayo ni watoto wetu hasa. Ni muhimu teknolojia hiyo itakuwa msaada kwao na si uangami-vu.

Hata kama tunaona tunakosa ujuzi wa kutosha, ni muhimu sisi wazazi tu-fungue milango ya maongezi na kuongea na watoto wetu. Hata kama tumeshindwa kuwashauri kamili, tunaweza kukaa nao tukiangalia kwa pamoja mambo hayo mapya, kuongea nao juu ya maoni yao na ya kwetu, na kuwauliza jinsi wanavyo-jisikia na kufikiri. Kwa pamoja, na chini ya maombi juu ya uongozi na ulinzi wa Mungu, inawezekana kusonga mbele.

### Kutiwa nguvu mpya

Ni wazi kuwa katika ulimwengu wa leo suala la matumizi ya teknolojia haliepuki-ki. Tukifikiri hatuhusiki tunajidanganya

wenyewe. Dunia ya leo inaendeshwa na utandawazi karibu kwenye kila eneo.

Lakini samaki wanaoelea na mkondo wa maji ndio wale tu waliokufa. Tunapochoka kwa sababu ya mawimbi ya mambo mapya kutufurika kila wakati, Mungu anatutia nguvu mpya kwa njia ya neno lake. Mwimba zaburi anasema neno la Mungu ni taa (Zab 119:105).

Maana yake hasa ni kwamba kila wakati linatuonesha hatua inayofuata kwenye njia ya kweli. Kama tukiliweka neno la Mungu moyoni mwetu na kulifuata kwa vitendo, inawezekana kuishi maisha na Mungu yaliyo safi (Zab 119:9-11).

Tunaposhindwa kujua jinsi ya kulinda familia yetu dhidi ya athari zilizo kwa sababu ya watu kutumia vibaya fursa zilizoletwa na teknolojia mpya, Mungu anatukaribisha kwake, akisema tusijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, tumjulishe haja zetu.

Mungu haahidi kwamba changamoto na matatizo yote yatatoweka papo hapo, bali anasema kwamba amani yake, ipitayo akili zote, itatuhifadhi mioyo yetu na nia zetu katika Kristo Yesu (Flp 4:6-7).

Basi, tumia nia yako hiyo kwa ajili ya kupanga kufanya mambo unayoona yata-faa familia yako na kuiletea baraka. Siyo tu kwamba muda wako kwa kuangalia mambo yote unayoona ni athari mbaya ya teknolojia unapungua unaposhughulisha mwili wako na akili yako kwa kutenda mema, Zawadi ya ziada itakuwa kwamba utafurahisha familia yako na kumvuta kila mmoja kufanya vivyo hivyo. Hata furaha yako mwenyewe itaongezeka.

.....  
Agape T. Mnzava na Philip Bach-Svensen

## Mwanamke Msamaria: Yesu ndiye njia ya uzima

Baada ya Samaria kuangukia katika miko-no ya mfalme wa Ashuru, mfalme huyo alileta watu wa mataifa na kuwamilikisha miji ya Samaria. Kwa sababu watu hawa hawakumcha Bwana, alipeleka simba kati yao. Basi, waliomba na kupewa kuhani Mwisraeli ili awafundishe imani ya Israeli, lakini matokeo yake haya-kuwa mazuri. Si utaifa tu uliochafuka lakini hata dini ya kweli (soma zaidi katika 2 Fal 17:24-41).

Kwa sababu hii Wayahudi wengine, hasa wa Yuda, waliwadharau Wasamaria, kwani li-

cha ya kutokuwa Wayahudi kamili, hawakufuata dini ya Kiyahudi kikamilifu. Wakihisi kudharauliwa, Wasamaria nao walipuuza mji wa Yerusalemu kama kitovu cha ibada za Wayahudi, na badala yake wakaufanya mlima Gerizimu kuwa mahali pao pa kuabudia (Yn 4:20).

Wayahudi walifanya kila juhudi kuchangamana na Wasamaria. Hata wengi wao wasingepitia nchi ya Wasamaria kwa kuogopa kunajisika. Lakini siku moja Yesu alipotoka Yuda kuelekea Galilaya, aliamua kupitia Samaria, na huko akakutana na mwanamke Msamaria kisimani kwa Sikari (Yn 4:3-6).

### Mwanamke wa aina gani?

Kuna habari inayodokeza kwamba pengine mwanamke huyu aliishi maisha ya ukahaba na kudharauliwa (4:17). Pengine hiyo ni sababu iliyomfanya kwenda kisimani kuteka maji pekee yake, saa sita

mchana, kinyume na desturi ya wanawake kwenda kisimani asubuhi au jioni.

Myahudi wa kawaida asingeegea na mwanamke kama huyu (4:9). Lakini Yesu aliongea naye!

Mwanamke Msamaria alifahamu mengi kuhusu ibada. Hata inaweze-lakini kwamba aliabudu. Lakini pamoja na hayo aliishi maisha ya dhambi. Inawezekana aliridhika kwamba njia iwe ile inayopitia Yerusalemu au hii ya Wasamaria iliyopitia kwenye mlima Gerizimu, barabara zote za ibada

zingeweza kumfikisha mtu kwa Mungu (4:20). Maana ya imani hiyo ni kwamba dini zote ni sawa, na mwisho wa zote ni wokovu.

Katika mazungumzo yao, Yesu alimsaidia mwanamke huyu kutambua kwamba Mungu hawatafuti wanaoabudu *mahali* fulani (k.m. Yerusalemu au Gerizimu), bali ataka sisi sote tumwabudu katika *roho na kweli* (4:23).

### Yesu ni nani?

Hii inamaanisha nini? Ina maana kwamba dini ni mpango wa mwanadamu kumtafuta Mungu, lakini wokovu uletao ondoleo la dhambi na uzima ni mpango na kazi ya Mungu katika kumtafuta mwanadamu.

Haikutosha kwa mwanamke huyu kufahamu kuwa Masihi alikuwa yuaja na kuwafunulia njia ya wokovu (4:25). Wala hakuwa na haja ya kuendelea kumsubiri,

Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! Haimkini huyu kuwa ndiye Kristo? (Yn 4:29)

kwani mbele yake tayari Masihi alisimama akiwa na kipawa cha maji yanayomaliza kiu ile inayotokana na dhambi na kuleta uzima wa milele (4:13, 26).

Ili kupokea msamaha wa dhambi na uzima wa milele, mwanamke Msamaria alihitaji kujitambua kuwa mwenye dhambi. Alikuwa ameishi na waume watano, na wa sita aliyekuwa naye hakuwa mumewe wa ndoa (4:17-18). Baada ya kufunuliwa hali yake ya dhambi na kutiwa tumaini kwamba amekutana na Kristo awezaye kumwokoza kutoka katika hali hiyo, mwanamke Msamaria aliuacha mtungi wake na kukimbia hadi kijijini akisema, “*Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! Haimkini huyu kuwa ndiye Kristo?*” (4:29)

Mwanzo wa mazungumzo yao, mwanamke Msamaria alikuwa amemtambua Yesu kuwa Myahudi tu. Baadaye alitambua kuwa aliyeongea naye alikuwa nabii. Kisha alimtambua kuwa Masihi na Kristo. Na haikuchukua muda yeye kutambua vilevile kwamba huyo Myahudi, huyo nabii, huyo Kristo, ndiye pia “Mwokozi wa ulimwengu” (4:42).

Alipofika kijijini na kueleza alivyoangaziwa dhambi zake na Yesu, Wasamaria wengi walitamani kusikia ujumbe wa Yesu, wakamsihi akae nao. Naye akakaa kwao kwa siku mbili (4:40). Na baada ya siku hizi mbili, Wasamaria wengi walimwamini Yesu. Siyo tu kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke Msamaria, lakini hasa kwa sababu wao wenyewe walithibitisha kwa hakika kwamba, huyu aliyeongea nao ndiye Kristo na Masihi wa Mungu, Mwokozi wa ulimwengu na njia pekee ya wokovu.

### Njia pekee ya uzima

Sawa na nyakati za mwanamke Msamaria, leo kuna dini nyingi sana, na kila mfuasi anafuata dini yake akiamini ndiyo njia sahihi. Husema, “Wewe una dini na mimi nina dini; fuata dini yako, nami nitafuata dini yangu, tukutane mbinguni.”

Inawezekana ndivyo alivyoamini mwanamke Msamaria. Ila wakati imani zilizobuniwa na wanadamu ni nyingi, Mungu wa Biblia ameidhinisha moja tu. Huu ndio mpango wake mwenyewe. Vilevile, ingawa wanadamu wamebuni njia nyingi za kutafutia msamaha wa maovu yao, kuna moja tu ya kuosha dhambi zetu. Ndiyo hiyo aliyoitoa Mungu. Inamaliza tatizo la dhambi zetu na kutupatanisha naye.

Yesu Kristo peke yake ndiye aliyetoka mbinguni. Anaitwa Masihi, Kristo wa Mungu, Mwana wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu (Lk 1:32, 2:11; Yn 3:16). Yesu Kristo ndiye, yeye peke yake, mpatanishi mkamilifu aliyetosha kutoa dhambi hu ya kukubalika mbele za Mungu (Ebr 7:25-28). Yesu Kristo ndiye, yeye peke yake, dhambi inayotosha kufidia dhambi zetu (Ebr 10:4, 10; Mk 10:45; Yn 1:29).

Hivyo Yesu Kristo siye moja wapo ya majina, au moja wapo ya dhambi, au moja wapo ya njia. Mungu amemwadhimisha na kumfanya jina la pekee litupasalo sisi kuokolewa kwalo (Mdo 4:12). Amemfanya kuwa dhambi pekee itoshayo kutupatanisha na Mungu, na njia pekee ya wokovu na uzima wetu (Yn 14:6).

.....*Mch. Gideon Mumo*

## Nimerudi na makovu, tena mtupu

Kwa muda wa miaka kadhaa nimekuwa mtu wa kutangatanga. Kiimani mimi nimekulia kwenye kanisa la Kilutheri. Wazazi wangu walinilea katika misingi mizuri ya kumpenda Mungu na kulipenda kanisa. Nilibatizwa nikiwa mdogo, nikapata kipaimara na kuendelea kuwa Mlutheri.

Baada ya kumaliza shule kidato cha sita nilianda chuo. Katika mwaka wangu wa kwanza bado nilianda ibadani kama kawaida. Lakini baadaye nilianza kuona kwamba ibada ya Kilutheri hazina zile amsha amsha kwangu kama kwa wengine. Kwa hiyo nilianza tabia ya kwenda Lutherani ibada ya kwanza, yaani ya saa moja, na mara tu baada ya mahubiri na kutoa sadaka nilitoka ibadani na kwenda kwingine ambako niliamini kulikuwa na amsha amsha za kutosha. Hali hii iliendelea kwa muda mrefu.

Kwa nini sikuacha kwenda Lutherani moja kwa moja? Kwa sababu niliamini kuwa wana utaratibu mzuri wa kutoa huduma pindi unapofikwa na tatizo kama kubatiza, misiba n.k. Kwa hiyo huku nilikuwa naenda ili nitambulike kuwa ni msharika aliyeandikishwa, lakini kiuhalisia sikuwa msharika bali mpitaji tu ambaye alikuwa anatengeneza mazingira ili apate huduma bila shida kama akitaka kubatiza mtoto, kufunga ndoa au huduma nyinginezo za kichungaji.

Huko nilikokuwa naenda nilikutana na nabii mmoja ambaye alikuwa ameanzisha huduma yake mwenyewe. Mwanzoni niliona niko salama. Kwa kuwa hali yangu ya kiuchumi ilikuwa nzuri, nilipata nafasi ya kuwa karibu na nabii wa kanisa lile. Hata hivyo nilijitahidi sana asijue

kwamba huwa naanzia ibada Lutherani, kisha naenda kwake.

Baada ya kusali kule kwa miaka miwili na nusu, siku moja nabii aliniita ofisini kwake na kuniambia ana mazungumzo nami. Nilitii na kwenda ofisini kwake. Katika mazungumzo yake aliniambia maneno ambayo yalinishtua na kuniogopesha sana. Aliniambia ameona nyota yangu inang'aa sana, lakini mume niliyekuwa naye siye mtu sahihi kwangu. Alieleza kuwa mume wangu alikuwa anazuia mafanikio yangu kwa sababu nyota yangu na nyota yake haziendani. Nilishtuka na kumwuliza nabii, Napaswa kufanya nini sasa? Naye alijibu kuwa sitafanikiwa kama nitaendelea kukaa na mume wangu ambaye nyota yake na yangu haziendani.

Kwa kweli sijui nini kilitokea, lakini nilijikuta ghafla nimeingiwa na hasira ya kumchukua mume wangu ambaye tumefunga naye ndoa na tumebarikiwa kuwa na watoto watatu. Na kwa kuwa mimi nilikuwa na kazi nzuri yenye mshahara mkubwa kuliko mume wangu, niliona naweza kufanya maamuzi yoyote na yeye asifanye lolote.

Katika mazungumzo yetu na nabii aliniambia wazi kwamba niachane na huyo mwanaume, kwani Mungu ameniandalia mume mwingine ambaye nyota zetu zinaendana. Kweli, baada ya miezi mitatu niliachana na mume wangu, na nabii alinitafutia nyumba eneo jirani na kanisa liliko. Wakati huu hata kule Lutherani nilikuwa nimeshaacha kwenda.

Nakumbuka siku moja nabii aliniambia atanifanyia maombi ya ukombozi. Maombi haya aliniambia yatafanyika

baada ya mfungo wa siku saba. Siku ya maombi ilipowadia nilianda kwa nabii huyu, na ilikuwa ni majira ya saa tatu usiku. Nilipofika pale nabii aliniambia maombi yale yatahusisha kupakwa mafuta mwili mzima. Wakati huo tulikuwa wawili tu ofisini kwake. Kwa kuwa niliamini ni mtumishi wa Mungu sikuwa na wasiwasi.

Mle ofisini kwake alikuwa na taulo jeupe akaniambia nivue nguo zote nijifunge taulo. Baadaye alichukua mafuta na kuanza kunipaka huku akinena. Huduma ile ya kupakwa mafuta iliendelea kwa muda na baada ya hapo sikumbuki nini kiliendelea. Ninachokumbuka ni kimoja tu, kwamba niliporudi kwenye ufahamu wangu wa kawaida nilikuwa ninafanya ngono na nabii. Kuanzia hapo niliendelea kulala na huyu nabii kama mume na mke. Sikukumbuka tena mume wangu, na mbaya zaidi, hata watoto wangu niliwasahau kabisa. Katika hayo yote hakuwa na mtu mwingine aliyekuwa anajua kinachoendelea isipokuwa mimi na nabii tu.

Baada ya mwaka mmoja wa mahusiano na huyu nabii, siku moja aliniambia anataka kuomba fedha zangu ili ziongezeke. Kwa hiyo nilianda benki kutoa fedha zangu zote zaidi ya milioni thelathini na tano na kumpatia nabii ili aziombe, kisha nianze biashara ya kuuza vitenge. Nafikiri kati ya makosa ambayo niliwahi kufanya maishani hili ni mojawapo. Yule nabii aliniambia kuwa baada ya siku 40 fedha zitakuwa zimebarikiwa, na akifanya biashara zitaongezeka.

Siku hiyo pia alinipaka mafuta, kisha nikalala naye kama kawaida, kisha akaniaga kuwa atasafiri safari ya siku 40 kwa ajili ya kutafuta faragha na Mungu, kisha baada ya siku hizo atarudi. Sikuwa na wasiwasi wowote, maana kwanza nili-

mwamini kama mtumishi wa Mungu, na pili kama mtu wangu wa karibu.

Niliendelea kukaa na kusubiri kwa amani kuwa mtumishi wa Mungu atarudi na fedha zangu zikiwa zimebarikiwa na kuongezeka. Lakini cha kusikitisha, hajawahi kurudi hadi leo hii, na umekwenda muda wa zaidi ya mwaka na nusu. Nilijaribu kufuatilia pale kanisani, kumbe sikuwa peke yangu niliyambiwa hivyo na nabii, hata tulikuwa wengi ambao tumetapeliwa. Kumbe yule bwana hakuwa nabii, bali alikuwa tapeli ambaye alitumia dini kututapeli. Na alipotimiza lengo lake akarudi kwao Nigeria. Kwa sasa hakuna tena kanisa pale wala ibada.

Kwa kweli nimedanganywa nikadangananyika. Kuna wakati ambao Mungu anaweza kutufundisha kupitia njia ngumu sana. Baada ya haya yote niliamua kurudi nyumbani kwenye dhehebu langu mama. Nilipofika huko nilimwambia mchungaji wangu yote, nikatubu na kurudi kwa Yesu. Kweli nimerudi, lakini nimerudi na makovu, tena kama mtu mtupu.

Najuta nilivyopoteza muda, utu wangu na hata fedha zangu kwa ulaghai wa kidini. Nimejifunza kuwa nyakati hizi ni mbaya. Afadhali kubaki uliko badala ya kutangatanga, maana matokeo yake kwangu ni kwamba nimekosa vyote. Yaani, nimekosa mume, watoto na nimepoteza takribani kila nilichokuwa nacho.

Kwa sasa nimebaki na mshahara tu bila akiba yoyote lakini moyoni nina amani ya Kristo kwa maana nina uhakika nimetubu na nimesamehewa. Na nimeona Mungu akinibariki kwa hiki kidogo ninachopata sasa.

*Mwenye ushuhuda huu anataka jina lake lisitajwe, lakini anafahamika na kamati ya Riziki*

# Bwana Anakuja

Kipindi cha majilio kinatupa sisi kama kanisa nafasi ya kuamsha hamu ya kumngojea Bwana wetu Yesu Kristo. Hiki ni kipindi cha upendo, matumaini, furaha na amani inayobubujika kutoka kwa Kristo Yesu kwa kanisa lake. Tunapata nafasi ya kuomba, kuimba nyimbo nzuri, na kufanya ibada mbali-mbali zinazohuisha ile hamu ya kumwona Bwana.

Wimbo unao-tusaidia kufanya hivyo ni namba 10 katika kitabu cha *Tu-*

*mwabudu Mungu Wetu*. Unaitwa *Bwana Anakuja* na kuimbwa sana wakati huu wa majilio.

Kanisa linapaswa kuwa tayari wakati wowote kumpokea Kristo, hivyo maandalizi lazima yafanyike ili anapokuja tuweze kumlaki. Wakristo tujifunze kufuata mfano wa wale wanawali wenye hekima waliojaza vyombo vyao mafuta wakimgoja Bwana Harusi na hivyo kuepuka kufanya kosa lile walilofanya wale wanawali wajinga waliokuta kwamba taa zao zimezimika. Soma Mt 25:1-13.

Wimbo huu *Bwana Anakuja* unatualika sote kumpokea Bwana kwa furaha, ukitukumbusha ni nani huyo tunayempokea, na ni nini alichobeba kwa ajili


yetu: *Bwana anakuja twendeni kumlaki, Bwana Mungu wa majeshi. Iwasheni mioyo tukampokee, huyu Mwenye utukufu.*

Bwana huyu *Mwenye utukufu* ndiye mfalme, ambaye akija kwetu, anatupa mahitaji yetu. Anatulisha kimwili na kiroho.

Haja yetu kuu ni nini hasa? Katika fungu la pili tunaimba, *Wewe ndiwe Mfalme, Mfalme wa mbinguni, utulisha wenye njaa. Wewe ndiwe mwanga, sisi tu vipofu, tufanye tuone tena.* Wimbo unatukumbusha Biblia inavyosema katika Zab 119:105, *“Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu”*.

Yesu anapokuja ndani yetu, anatupa mwanga wa kutuongoza siku zote katika maisha yetu. Katika dunia hii iliyojaa mambo maovu na nguvu za giza zinazotafuta kuwaangamiza watu, kukaa katika mwanga wa Yesu ndiyo siri ya ushindi na wokovu kwetu.

Ubeti wa tatu unatukumbusha Yesu anavyojitambulisha katika Yn 14:6, *Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.* Tunamtukua Yesu katika wimbo huu kama njia tukimpa ahadi ya kumfuata ili tusi-



potee bali atupeleke kwa Baba yetu Mbinguni: Wewe ndiwe njia, tutakufuata, turudi kwa Baba yetu. *Wewe ndiwe kweli, utuangazie, tusije tukapotea.* Wakristo tupo safarini kwenda Mbinguni kwa Mungu, hivyo ni muhimu kukaa katika njia ili tusipotee. Njia hiyo ni Yesu.

Ubeti wa nne unajenga katika habari njema ya Yesu kuwa mkombozi wa ulimwengu. Kuja kwake kwetu kunatupa *matunda ya ukombozi*, ambayo ni pamoja na kutoka katika utumwa na vifungo vya shetani. Yesu ni mbarikiwa, na hivyo anatubariki sisi. Baraka kubwa kuliko zote ni kwamba tunaweza kufurahia kuwa pamoja naye kwa kuwa tumekombolewa: *Hosana, Hosana, huyo mbarikiwa, anakuja*

*kwetu sisi. Aja kutulisha na kutugawia matunda ya ukombozi. Karibu, Bwana, njoo. Shinda pamoja nasi.*

Kiitikio hiki, *Karibu Bwana, njoo. Shinda pamoja nasi*, kinatukumbusha kumkaribisha huyo Mfalme anayekuja kwetu ili akae nasi muda wote. Kumpokea ni pamoja na wajibu wa kuzungumza naye, na kumsikiliza anayotufundisha. Lakini kwanza na hata mwisho ni kukaa katika ushindi wake.

Huu wimbo mzuri sana umetungwa na Moses O. M. Mdegella. Tuuimbe kwa furaha wakati wote tukitafakari ujumbe wake, ili huu utusaidie kujiweka tayari kila wakati kumpokea Bwana.

.....  
*Cathbert Msemo*

## BWANA ANAKUJA

1. Bwana anakuja twendeni kumlaki, Bwana Mungu wa majeshi. Iwasheni mioyo tukampokee, huyu Mwenye utukufu.

*/: Karibu Bwana, njoo :/  
Shinda pamoja nasi.*

2. Wewe ndiwe Mfalme, Mfalme wa Mbinguni, utulisha wenye njaa. Wewe ndiwe mwanga, sisi tu vipofu, tufanye tuone tena.

3. Wewe ndiwe njia, tutakufuata, turudi kwa Baba yetu. Wewe ndiwe kweli, utuangazie, tusije tukapotea.

4. Hosana, Hosana, huyo mbarikiwa, anakuja kwetu sisi. Aja kutulisha na kutugawia matunda ya ukombozi.

# Anza yote na Bwana

Sisi sote tunapanga malengo mengi ya maisha, na tukiri tu kwamba kweli tunasumbuka na utekelezaji wake. Lakini tunajifunza nini kwa kusumbukia maisha?

Yesu katika mafundisho yake kwa wafuasi wake aliwaambia kwamba kamwe wasiwasi hauwezi kuzaa matunda mazuri. Kuwa na wasiwasi katika maisha hakujawahi kuwa na tija. Hata hutuzuia kutimiza makusudi ya ufalme wa mbinguni ambao ametuitia.

”Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili ... Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?” (Mt 6:25)

Je, Yesu hataki tuwe na malengo katika maisha, wala kujali tunakula na kunywa nini? Anamaanisha nini anaposema msisumbukie maisha? Jibu lake liko wazi, “Utafuteni kwanza ufalme wake [Mungu], na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa” (Mt 6:33). Tutafakari maana yake.

## Tutafuteje vilivyo vya Mungu?

Jambo la kwanza ili tuweze kuatafuta ufalme wa Mungu ni kumjua Mfalme. Ufalme wa Mungu ulikuja kupitia Yesu. Lazima tumfahamu Yeye kwanza, na haki yake, maana Yesu ndiye mfalme anayetajwa.

Kuatafuta kwanza ufalme wa Mungu, maana yake ni kuwa na Yesu kama mtawala na kiongozi wa maisha yetu. Kwanza na hata mwisho hii ni sawa na kutafuta uhusiano naye, na kujiweka wazi kwake. Inajumuisha kujitiisha katika mamlaka yake, kuishi kulingana na mafundisho

yake, na pamoja na wote waaminio kutanguliza utawala wa Mungu kwa kutumikia kuenea kwa ufalme wake hapa duniani.

Je, tunamtanguliza Mungu katika maisha na mipango yetu? Kuna watu wengi wanaomwendea Mungu ili kupata faraja, nguvu, au mahitaji mengineyo, lakini hiyo siyo kufanya kama Yesu anavyosema.

Mungu anataka yeye mwenyewe awe na nafasi ya kwanza, kabla ya malengo mengine yote. Yeye awe ni wa kwanza, tena awe yote katika yote. Katika Kut 20:3 aliweka jambo hili wazi akiwaambia wana wa Israeli kuwa wasiwe na miungu mingine ila Yeye. Awe ndiye Mungu pekee maishani mwetu (Kut 20:3).

Tunamtanguliza Mungu pale tunapomtegemea yeye kuliko sisi wenyewe, au mtu mwingine au kitu kingine chochote. Bila shaka ni pamoja na kumwabudu Mungu, kumsifu, kumshukuru na kutumikia mapenzi na mipango yake.

## Usipange peke yako

Hatuwezi kutenga chochote katika maisha yetu Mungu asikitawale, maana anatumia hali zetu zote ili kutimiza makusudi yake, na anataka tumwamini na kuungana naye katika hilo.

Je, Yesu ana nafasi gani wakati wewe unapanga malengo na mipango yako?

Kumbuka alisema, “Utafuteni kwanza ufalme wake” Mungu. Malengo yasiyo na msingi wa Mungu hayana mafanikio ya kudumu. Mtu anayetafuta kweli ufalme wa mbinguni, hawezi kupanga akiwa peke yake. Lazima Yesu awepo kama wa kwanza na mwenye uamuzi.

Tuko wengi tulio na malengo na mipango mingi katika maisha yetu. Mwaka baada ya mwaka tunaweka hayo malengo. Shida ni kwamba mara nyingi tunaanza na mawazo yetu, kisha tunamshirikisha Mungu ili ayafanikishe. Au tunakwenda kwa Mungu baada ya kushindwa sisi wenyewe kufikia malengo tuliyojiwekea, tukifanya maombi na dua za kulalamika kwa nini Mungu hajatafanikisha.

Kumbuka siku zote Mungu ana mpango kamili wa maisha yako. Yeye anasema anajua mpango anaotuwazia, tena ni mpango mzuri na wa amani, ili atupe matumaini katika nyakati zetu za mwisho (Yer 29:11). Kwa hiyo sisi kupanga wenyewe mipango nje ya mpango huo wa Mungu ni kupoteza mwelekeo wa kule Mungu alikotupangia kufika.

Kama yeye ana mpango huo na maisha yetu, ni kwa nini basi tusumbuke na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi?

## Malengo yasikinazane na mpango wa Mungu

Hakuna anayejua mipango yote ya Mungu kwa maisha yake, lakini lengo lake kuu ni wazi: Ni kukusogeza karibu na Yesu, Mfalme wa ufalme wa mbinguni. Hivyo tuna uhakika juu ya mwelekeo katika mipango yake yote.

Kwa mfano, una malengo gani katika kulinda afya yako ya kiroho? Kama ukitafuta kwanza ufalme wa Mungu, jibu la swali hili linatarajiwa kuwa pamoja na ratiba nzuri ya kusoma Biblia, binafsi na kifamilia, na kawaida ya kukusanyika na waamini wengine katika ibada na mikusanyiko ya kiroho, maana ni kupitia njia hizo tuko pamoja na Mungu, na yeye anatuongoza.

Pili, utakuwa na malengo gani katika kuutunza mwili wako? Yesu anaposema tusisumbuke kuhusu kula na kunywa, maana yake siyo kutokujali mahitaji ya mwili. Kama ukitafuta kwanza ufalme wa Mungu, utakuwa mwangalifu kwenye vyakula unavyokula na vinywaji unavyokunywa. Pia utakuwa na nidhamu katika kufanya mazoezi ya mwili pamoja na kuhakikisha unakuwa na muda mzuri wa kulala.

Wengi wetu hatuna nidhamu ya kutunza miili yetu. Tunakunywa maji tukisikia kiu, hatunywi kama hitaji muhimu la mwili. Hatufanyi mazoezi, na tunalala kwa kuchelewa mno. Lakini usipotunza afya ya mwili wako, kuna uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa mbalimbali na hivyo kushindwa kuyatimiza hata hayo mengine yanayohusiana na mipango ya Mungu kwa maisha yako hapa duniani.

## Malengo ya familia yako

Tuko wengi tulio na malengo makubwa ya kutafuta kufanikiwa. Kwa hiyo tumejipanga kufanya kazi kwa bidii ili kwa njia zozote zile kuhakikisha mambo yetu yanafanikiwa. Lakini katika bidii yetu mara nyingi kuna lengo moja muhimu tunalotaka kulisahau: Unapanga malengo gani kuhakikisha familia yako inakuwa familia bora?

Kuna tofauti kubwa kati ya kuwa na familia tajiri na familia bora. Unaweza ukawa na familia tajiri, lakini siyo bora. Ukilizingatia hili utawekeza sana katika kuwa karibu na familia yako. Utahakikisha watoto wako wanapata mahitaji yao muhimu ya kiroho, kimwili na kijamii.

.. inaendelea uk.16



.. kutoka uk.15

Familia bora yenye malezi mazuri inatambua kuna majira na nyakati katika maisha. Inajua kuwa na kitu, na pia kupungukiwa nacho. Inajua kushiba, na inajua kuwa na njaa. Katika familia ya namna hii ni rahisi kukaa chini na kupanga malengo ya baadaye ya maisha ya kila mmoja. Familia ya namna hii inajua wapi pa kuweka vipaumbele hata katika matumizi yake.

### **Weka malengo ya kuwekeza**

Wengi tunafanya kazi kwa bidii, iwe ni maofisini, mashambani, kwenye biashara n.k, lakini hatuna nidhamu ya kuwekeza. Tunakula kila kitu tunachopata kana kwamba tutanyakuliwa kesho. Hii si maana ya neno la Yesu akisema, “Msisumbukie ya kesho” (Mt 6:34), maana anachotuonya si kuwekeza bali kusumbuka.

Jiwekee malengo ya kuwekeza pamoja na kutegemea kwamba Baba yako wa mbinguni anajua mahitaji yako yote. Hakuna akiba ndogo ikiwekwa kwa uaminifu. Maisha yetu yana kupata leo na kukosa kesho. Utakapokosa kesho, au yakitokea mambo kama yale ya kipindi cha covid-19 ambapo kukawa hakuna

kutoka wala kufanya kazi, je, utakuwa na akiba ya kuendesha maisha?

### **Fanya tathmini**

Baada ya kufuata malengo fulani kwa muda, ni vizuri kukaa chini na kufanya tathmini umefanikiwa kwa kiasi gani. Huwezi kusema umefanikiwa ikiwa hujafanya tathmini ya kile ulichokuwa umepanga na jinsi ulivyopanga kukitekeleza. Angalia yaliyofanikiwa, na yale ambayo hayajafanikiwa, kisha jiulize kwa nini haya lakini si yale. Hii itakusaidia kufanya mpango mzuri siku nyingine na kukulinda usirudie makosa yaliyopita.

Kumbuka tena na tena, Mungu ni namba moja! Basi mwombe achukue nafasi hiyo kwenye kila unalopanga. Yeye mwenyewe, yeye peke yake ni ulinzi dhidi ya wasiwasi na masumbuko yote. Fuata mapenzi yake kwa afya yako ya mwili, akili na roho. Nje ya hapo ungekuwa na malengo mengi, lakini mwisho wa hayo yote utalazimika kukubali kwamba jiti-hada zako zote zilikuwa bure.

*James Sabuni*

**SOMA BIBLIA**

0759 544 917

S.L.P. 2696, Arusha

editor.somabiblia@gmail.com

www.somabiblia.or.tz



Soma RIZIKI “online”

www.issuu.com/riziki